**HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KWENYE DHIFA YA KITAIFA ILIYOANDALIWA NA MHESHIMIWA EVARISTE NDAYISHIMIYE, RAIS WA JAMHURI YA BURUNDI BUJUMBURA, TAREHE 16 JULAI, 2021**

***Mheshimiwa Evariste Ndayishimiye, Rais wa Jamhuri ya Burundi pamoja na Mama Ndayishimiye;***

***Waheshimiwa Mawaziri wa Tanzania na Burundi mliopo;***

***Viongozi wengine wa Serikali zetu mbili mliopo;***

***Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Taasisi za Kimataifa;***

***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana:***

Nianze kwa kurudia kukushukuru sana kaka yangu, Mheshimiwa Rais Evariste Ndayishimiye kwa kunialika kutembelea nchini mwako. Aidha, kwa mara nyingine tena, nakushukuru wewe binafsi, Serikali pamoja na Wananchi wa Burundi, hususan Wakazi wa Jiji hili zuri la Bujumbura, kwa mapokezi yenu mazuri mazuri. Kwenye Uwanja wa Ndege nilipokewa na Makamu wa Rais, lakini njiani kote nilikopita wana-Bujumbura walijitokeza kwa wingi kunilaki. Kwa hakika nakosa

neno zuri la kuelezea shukran zetu kwenu zaidi ya kusema ***"Murakoze Chaane"***.

Napenda pia kutumia fursa hii kukushukuru kaka yangu, kwa maneno mazuri uliyoyasema kunihusu mimi pamoja na nchi yangu ya Tanzania. Kwa niaba ya Watanzania wote, tunasema ahasante sana. Lakini nataka niseme kuwa, mimi na wewe tumechukua dhamana ya kuongoza Mataifa yetu katika mazingira yanayofanana kiasi. Baada ya vifo vya Watangulizi wetu. Tofauti tu ni kwamba, wewe mwenzangu tayari ulishachaguliwa kuwa Rais na hivyo ulikuwa ukisubiria kuapishwa; wakati mimi nimechukua Uongozi nikiwa Makamu wa Rais. Lakini, sote hatukupata bahati ya kukabidhiwa Uongozi na Watangulizi wetu.

Hivyo basi, nitumie fursa hii, kukupongeza sana kaka yangu kwa kazi kubwa uliyoifanya tangu umechukua dhamana ya kuiongoza Burundi. Katika kipindi kifupi cha Uongozi wako, umeimarisha amani na usalama, umeanzisha mageuzi ya kiuchumi na kijamii, umeongoza mapambano dhidi ya rushwa na umeimarisha uhusiano na nchi pamoja na taasisi za kimataifa. Na katika hilo, Tanzania tunaendelea kutoa wito kwa nchi pamoja na

taasisi za kimataifa ambazo bado hazijaondoa vikwazo kwa Burundi, kufanya hivyo.

***Waheshimiwa Viongozi;***
***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Kuna usemi unasema, *"Unaweza kuchagua rafiki, lakini huwezi kuchagua jirani"*. Usemi huu una maana kuwa, unaweza kuwa na jirani lakini asiwe rafiki yako. Tanzania na Burundi sisi ni majirani; lakini pia ni marafiki. Zaidi ya yote, sisi ni ndugu. Udugu na urafiki wetu umekuwepo tangu enzi na enzi, hata kabla ya mataifa yetu hayajapata uhuru. Mtakumbuka, kabla ya ukoloni, zilikuwepo baadhi ya tawala za kichifu ambazo zilitawala kwenye baadhi ya maeneo ya Tanzania na Burundi. Aidha, mtakumbuka kuwa, baada ya Mgawanyo wa Bara la Afrika mwaka 1884/85, Burundi, Tanganyika (hivi sasa Tanzania) pamoja na Rwanda ziliwekwa chini ya Himaya ya Ujerumani. Hii inathibitisha kuwa sisi ni wamoja. Ndiyo sababu, leo hii ukiienda Kabanga/Kobero au Manyovu/Mugina huwezi kujua yupi Mtanzania na yupi Mrundi.

Uhusiano na ushirikiano wetu ulimarika zaidi baada ya mataifa yetu kupata Uhuru, na hasa kwa kupitia Waasisi wetu,

Hayati Baba wa Taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Waziri Mkuu wa Burundi Prince Louis Rwegashore. Kupitia viongozi hao waasisi, nchi zetu ziliweza kushirikiana vizuri kitaifa, kikanda na kimataifa. Kwa bahati nzuri, Viongozi wa Awamu zilizofuatia waliendeleza uhusiano huo. Tumekuwa tukishirikiana nyakati za shida na raha.

Tanzania imeweka historia ya kuwapokea wakimbizi kutoka Burundi kufuatia matatizo yaliyotokea miaka ya 1970, 1990 na 2000. Tanzania pia ilisimamia mazungumzo ya amani ya Burundi yaliyopelekea kusainiwa kwa Mkataba wa Amani na Maridhiano ya mwaka 2000. Kama hiyo haitoshi, Tanzania imetoa urai kwa waliokuwa wakimbizi wa Burundi, hususan waliongia nchini mwaka 1972. Tulifanya hivyo, ili kutimiza wajibu wetu kama nchi lakini pia kwa kutambua kuwa sisi Watanzania na Warundi ni wamoja: ni ndugu, marafiki na majirani. Kama mnavyofamu, kwa mila na desturi zetu Wafrika, ndugu na majirani daima husaidiana. Tusingefanya hivyo au tusingejishughulisha na chochote kilichokuwa kikitokea Burundi, ulimwengu na wenye kufahamu historia yetu wasingetuelewa.

Na kwa msingi huo huo wa kusaidiana na kushirikiana nyakati za shida na raha, napenda kutumia fursa hii kurudia tena kuwashukuru ndugu, marafiki na majirani zetu wa Burundi kwa kuwa nasi kwenye vipindi vigumu ambavyo Taifa letu limepitia. Mathalan, mlitufariji sana wakati wa msiba mkubwa wa aliyekuwa Rais wetu, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli; lakini pia, tangu nimewasili Mheshimiwa Rais Ndayishimiye amekuwa akinipa pole kufuatia kuungua kwa Soko la Kariakoo. Hii inadhihirisha kuwa shida yetu ni shida yenu; na maumivu yetu ni maumivu yenu. Tunawashukuru sana.

***Mheshimiwa Rais Ndayishimiye;***
***Waheshimiwa Viongozi;***
***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Asubuhi nilisema nimekuja Burundi kwanza kujitambulisha rasmi kama Kiongozi mpya wa Tanzania. Kama mnavyofahamu, kwa utamaduni wetu Waafrika, ukiwa mpangaji mpya ama ukihamia katika mtaa ni lazima ujitambulishe. Pili, nimekuja Burundi kuwapongeza kwa mafanikio makubwa mliyoyapata, ambayo yamewawezesha kutoa mchango mkubwa kimataifa,

ikiwemo kuchangia vikosi vya amani nchini Somalia na Jamhuri ya Afrika ya Kati. Hongereni sana ndugu zetu wa Burundi.

Sababu ya tatu iliyonileta Burundi ni kuendeleza uhusiano na ushirikiano kati yetu. Kama nilivyosema awali, nchi zetu zina uhusiano mzuri sana. Hivyo basi, nimekuja Burundi kuhakikisha uhusiano wetu unaendelea kukua zaidi na zaidi. Na katika hilo, nimefarijika sana leo kwenye mazungumzo yetu, tumejadili kwa kirefu namna ya kukuza uhusiano na ushirikiano kati yetu, ikiwemo kuondoa vikwazo na kuimarisha miundombinu ili kukuza biashara na uwekezaji kati yetu.

Na katika hilo, nimefurahi, kwenye ziara hii nimepata fursa ya kumtembelea Mfanyabiashara wa Burundi, Mmiliki wa Kiwanda cha Mbolea ya Fomi, ambaye ameamua kuwekeza Tanzania kwa kujenga Kiwanda kama hicho pale Dodoma. Nataka nimwahakikishie mwekezaji huyo kuwa tutampa ushirikiano wa kutosha ili aweze kutimiza malengo yake. Leo pia nimepata ya kutembelea Tawi la Benki ya CRDB hapa Burundi ambayo ni Benki ya Kitanzania. Hii ndiyo haswaa diplomasia ya uchumi, ambayo kaka yangu Mheshimiwa Rais Ndayishimiye ameileza. Tumepata

pia fursa ya kugusia suala la *Corona*. Kama mjuavyo, janga hili halina mipaka na limeikumba dunia yote. Hivyo basi, tumejadiliana kuhusu namna ya kushirikiana katika kukabiliana na janga hilo, hususan katika maeneo ya mipaka yetu.

***Waheshimiwa Viongozi;***
***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Nimeangalia mpingilio wa meza hapa Ukumbini ni dhahiri kuwa kuna chakula kimeandaliwa. Na kwa mila na desturi zetu za Waafrika, wakati wa chakula sio wa kuzungumza. Hivyo basi, nihitimishe kwa kurudia kumshukuru Mheshimiwa Rais Ndayishimiye kwa kunialika. Namshukuru pia kwa makaribisho mazuri. Nataka nikuahidi kuwa Tanzania itaendeleza uhusiano mzuri na Burundi kwa manufaa ya nchi zetu mbili na watu wake.

Baada ya kusema hayo, naomba sasa, kwa heshima na taadhima, sote tusimame na kisha tunyanyue glasi zetu:

- ***Kwa ajili ya afya njema ya Mheshimiwa Evariste Ndayishimiye na Mama Ndayishimiye;***
- ***Kwa ajili ya urafiki na ushirikiano mzuri kati ya Tanzania na Burundi.***

**"AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA".**